



Nzalauka

Hukomaa baada ya miezi 6 hadi 8. Mavuno yake ni tani 21 kwa kila eka. Mizizi yake ina ngozi ngumu. Ina matawi imara, na haina tashuishi ikikuzwa pamoja na mimea mingine.



Karibuni

Hukomaa baada ya miezi 8 hadi 12. Mazao ni tani 21 kwa kila eka. Mizizi yake huwa na umbo la duara na ngozi yake ni ngumu. Matawi ni mafupi na yenye vijitawi vingi.

Eneo la kuzalisha mbegu

Kuandaliwa kwa mbegu za kupanda hufanyika KARI Mtwapa, Msabaha na Mpeketoni.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Watayarishaji:

Muli M.B., Saha, H.M., Shuma, J na Weru S.M.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Mtwapa

S.L.P. 16, Mtwapa, 80109

Simu/Nukulishi: 0202024751

Baruapepe: karimtw@kari.org

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 58 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Aina mpya za mihogo katika Pwani ya Kenya



Utangulizi

Wakulima wengi wa pwani ya Kenya hupanda mihogo ya kawaida ambayo hutoa mazao duni na husumbuliwa na maradhi. Magonjwa sugu katika sehemu hizi huwa virusi vya *cassava brown streak* na *cassava mosaic*.




Virusi vya Cassava mosaic

KARI-Mtwapa imeibuni aina sita za mihogo ya mazao ya juu yenye kustahimili maradhi sugu. Aina hizi zinaweza kutoa tani 20 hadi 28 kwa kila ekari, ikilinganishwa na aina ziliziko zenye mazao kati ya tani 4 hadi 14 kwa kila eka.



Virusi vya Cassava brown streak

Zifuatazo ni baadhi ya maumbile ya aina hizo za mihogo.



Shibe

Hukomaa baada ya miezi 8 hadi 12; Mavuno ya mizizi ni tani 28 kwa kila eka. Mizizi yake ni laini, yenye ganda la manjano na matawi yake ni imara bila vijitawi.



Tajirika

Hukomaa baada ya miezi 8. Mazao yake ni tani 25 kwa kila eka. Mizizi yake ni laini, mirefu, na yenye ganda nyeupe kiasi. Matawi yake ni imara.



Karembo

Hukomaa baada ya miezi 8. Mavuno ni tani 27 kwa kila eka. Ni fupi na mizizi yenye umbo lililotawanyika. Haifai kuchanganywa na mimea mingine.



Siri

Hukomaa baada ya miezi 8 hadi 12. Mazao yake ni tani 23 kwa kila eka. Ni fupi na haina matawi. Ina mizizi laini yenye kutawanyika.